# Baraka vs Laana katika maisha ya Mkristo

“Taifa” la BWANA la leo ni Kanisa Lake. Kanisa Lake limeenea dunia nzima, na halitakuwa na mwisho (Dan. 3:44; 6:26). Injili na neno la Mungu ndiyo njia ambayo Kanisa linaujenga na kuuendeleza ufalme wa BWANA. Injili inatumiwa na BWANA katika kuteua na kufundisha watumishi watakaolijenga Kanisa Lake (Matt. 29:18-20; Marko 16:15-16; Matendo 1:8); watumishi hawa walichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Matendo 13:48; War. 9:11-31).

Matendo 1:8 Lakini mtapokea uweza, Roho Mtakatifu atakapowajia; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi yote, na Samaria, ***na hata ncha za dunia***.

Matendo 13:48 Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana: ***nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini***.

**KUMB. 27:1-26**

Kumb. 27:1-8 ni aya zinazothibitisha AGANO kati ya Mungu na wana wa Israeli:

27:1 Musa na wazee wa Israeli wakawaagiza wale watu wakawaambia, Shikeni maagizo yote niwaagizayo leo.
2 Na iwe, siku mtakayovuka Yordani kwenda nchi akupayo Bwana, Mungu wako, ujisimamishie mawe makubwa, ukayatalize matalizo,
3 uyaandike maneno yote ya torati hii juu yake, utakapokwisha kuvuka; ili upate kuingia nchi akupayo Bwana, Mungu wako, nchi imiminikayo maziwa na asali, kama alivyokuahidi Bwana, Mungu wa baba zako.
4 Na iwe, mtakapokwisha vuka Yordani myasimamishe mawe haya, niwaagizayo hivi leo, katika mlima Ebali, nawe yatalize matalizo.
5 Na huko umjengee madhabahu Bwana, Mungu wako, madhabahu ya mawe, usitumie chombo cha chuma juu yake.
6 ***Jenga hiyo madhabahu ya Bwana, Mungu wako, kwa mawe yasiyochongwa; ukamtolee Bwana, Mungu wako, sadaka za kuteketezwa juu yake;***
7 ***ufanye na sadaka za amani, ukale huko; nawe furahi mbele za Bwana, Mungu wako***.
8 Kisha, andika juu ya mawe hayo maneno ya torati hii yote, waziwazi sana.

27:9 Musa na makuhani Walawi wakawaambia Israeli wote wakasema, Nyamaza, usikilize, Ee Israeli; leo umekuwa taifa la BWANA, Mungu wako.
27:10 Basi isikilize sauti ya BWANA, Mungu wako, ufuate amri na kanuni zake ninazokuagiza leo.

27:11 Musa akawaagiza wale watu siku hiyo hiyo, akasema,
27:12 Hawa na wasimame juu ya mlima wa Gerizimu ili kuwabariki watu, mkiisha vuka Yordani; Simeoni, na Lawi, na Yuda, na Isakari, na Yusufu, na Benyamini;
27:13 Na hawa na wasimame juu ya mlima wa Ebali ili kulaani; Rubeni, na Gadi, na Asheri, na Zabuloni, na Dani, na Naftali.
27:14 Kisha Walawi na wajibu, wawatamkie watu wote wa Israeli kwa sauti kuu,
27:15 Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya kuchonga, au ya kusubu, machukizo kwa Bwana, kazi ya mikono ya fundi, akaisimamisha mahala pa siri.
Na watu wote wajibu, waseme, Amina.
27:16 Na alaaniwe atakayemdharau baba yake au mama yake.
Na watu wote waseme, Amina.
27:17 Na alaaniwe atakayeondoa mpaka wa jirani yake.
Na watu wote waseme, Amina.
27:18 Na alaaniwe ampotezaye kipofu akakosa njia.

Na watu wote waseme, Amina.
27:19 Na alaaniwe atakayepotosha hukumu ya mgeni, na yatima, na mjane aliyefiwa na mumewe.
Na watu wote waseme, Amina.
27:20 Na alaaniwe alalaye na mke wa baba yake, kwa kuwa amefunua mavazi ya baba yake.
Na watu wote waseme, Amina.
27:21 Na alaaniwe alalaye na mnyama wa aina yo yote.
Na watu wote waseme, Amina.
27:22 Na alaaniwe alalaye na umbu (dada) lake, binti ya babaye, au binti ya mamaye.
Na watu wote waseme, Amina.
27:23 Na alaaniwe alalaye na mkwewe, mamaye mkewe.
Na watu wote waseme, Amina.
27:24 Na alaaniwe atakayempiga mwenzake kwa siri.
Na watu wote waseme Amina.
27:25 Na alaaniwe apokeaye ujira ili kumwua asiye na kosa.
Na watu wote waseme, Amina.
27:26 Na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii kwa kuyafanya.
Na watu wote waseme, Amina.

**KUMBU: MLANGO 28**

28:1 Itakuwa utakaposikia sauti ya BWANA, Mungu wako, kwa bidii, kufuata na kutenda maagizo yake yote nikuagizayo leo, ndipo BWANA, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani;
28:2 Na ***baraka hizi zote zitakuja kwako*** na zitakufikia usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako.
28:3 Utabarikiwa mjini, na utabarikiwa shambani.
28:4 Utabarikiwa uzao wa mwili wako, na uzao wa shamba lako, na uzao wa ng'ombe wako, ongezeko la fahali wako, na makundi ya kondoo zako.
28:5 Litabarikiwa kapu lako, na ghala lako.
28:6 Utabarikiwa utakapoingia ndani, utabarikiwa na utakapotoka nje.
28:7 BWANA atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako; watakuja dhidi yako kwa njia moja, lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.
28:8 BWANA ataamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na katika mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo BWANA, Mungu wako.
28:9 BWANA atakuweka uwe taifa takatifu kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya BWANA, Mungu wako, na kutembea katika njia zake.
28:10 Na mataifa yote ya duniani wataona kwamba umeitwa kwa jina la BWANA, nao watakuwa na hofu mbele yako.
28:11 BWANA atakufanya uwe na wingi wa mali, katika uzao wa mwili wako, na katika uzao wa ng'ombe wako, na uzao wa shamba lako, katika nchi ambayo BWANA aliapa kwa baba zako kwamba atakupa.
28:12 BWANA atakufungulia hazina yake njema, mbingu itanyesha mvua katika nchi yako kwa wakati wake, na kuibariki kazi yote ya mikono yako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala wewe hutakopa.
28:13 BWANA atakufanya uwe kichwa, na si mkia; nawe utakuwa juu tu, kamwe hutokuwa chini [ya yeyote], ikiwa utasikiliza maagizo ya BWANA, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyafuata na kuyatenda;
28:14 Msikengeuke katika haya ninayowaamuru leo, msiende kuume wala kushoto kwayo, kwa kuifuata miungu mingine na kuitumikia.

28:15 Lakini ikiwa hutomtii BWANA, Mungu wako, kwa kutofuata maagizo yake yote na amri zake ninazokuagiza hivi leo, ndipo ***laana hizi zote zitakuja kwako*** na kukufikia:
28:16 Utalaaniwa mjini, utalaaniwa na shambani.

28:17 Litalaaniwa kapu lako na ghala lako.
28:18 Utalaaniwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, ongezeko la ng'ombe wako, na makundi ya kondoo zako.
28:19 Utalaaniwa uingiapo ndani, utalaaniwa na utokapo nje,
28:20 BWANA atakuletea laana, maudhi, na kukemewa, katika yote utakayotia mkono wako kuyafanya, hata uangamie na kupotea kwa upesi; kwa ule uovu wa matendo yako, uliyoniacha kwayo.
28:21 BWANA atasababisha tauni isiondoke kwako, hata atakapokuondoa katika nchi uingiayo kwa kuimiliki.
28:22 BWANA atakupiga kwa kifua kikuu, na kwa homa, na kwa uvimbe, na kwa joto [kali], na kwa upanga, na kwa ukaufu, na kwa koga; navyo vitakuandama hata uangamie. (Matt. 24:7)

28:23 Na mbingu zako zilizo juu ya kichwa chako zitakuwa shaba, na nchi iliyo chini yako itakuwa chuma. ***NB: Mvua kutonyesha na ardhi kutolimika kwa ugumu wake. Haya yametokea hapa Tanzania.***
28:24 BWANA atafanya mvua ya nchi yako iwe vumbi na mchanga; itakuja juu yako kutoka mbinguni hata uangamie. ***NB: Mafuriko na gharika. Wenyewe tunaita El Nino!***
***Kwa hakika, matukio ya aya ya 23 na hii ya 24 tunayaita 'mabadiliko ya tabia nchi'!***

28:25 BWANA atakufanya upigwe mbele ya adui zako; utawatokea dhidi yao kwa njia moja, lakini utakimbia mbele yao kwa njia saba; nawe utatupwa huko na huko katika falme zote za duniani.
28:26 Na mzoga wako utakuwa chakula cha ndege wote wa angani, na wanyama wote wa duniani, pasiwe na mtu wa kuwafukuza. (Ufu. 19:17-19)
28:27 BWANA atakupiga kwa majipu ya Misri, na kwa bawasiri, na kwa upele, na kwa muwasho, ambayo hutopata kupoa.
28:28 Bwana atakupiga kwa wazimu, na kwa upofu, na kwa bumbuazi la moyoni;
28:29 Utakwenda kwa kupapasa-papasa mchana, kama apapasavyo kipofu gizani, wala hufanikiwi katika njia zako; nawe sikuzote utaonewa na kutekwa nyara, wala hapatakuwa na mtu wa kukuokoa.
28:30 Utaposa mke na mume mwingine atalala naye; utajenga nyumba usikae ndani yake; utapanda mizabibu usivune matunda yake.
28:31 Ng'ombe wako atachinjwa mbele ya macho yako, usile nyama yake; utanyang'anywa punda wako mbele ya uso wako kwa jeuri, usirudishiwe; kondoo zako watapewa adui zako, usipate mtu wa kuwaokoa.
28:32 Wanao na binti zako litapewa taifa lingine, na macho yako yataangalia, na kuzimia kwa kuwatamani mchana kutwa; wala hapatakuwa na kitu unachoweza kufanya juu ya hilo.
28:33 Matunda ya nchi yako, na kazi yako yote, vitaliwa na taifa usilolijua; utaonewa tu, na kukandamizwa daima;
28:34 Hata uwe mwenye wazimu kwa utakayoona kwa macho yako.
28:35 BWANA atakupiga katika magoti na miguu yako, kwa jipu kuu lisilopona, tokea unyayo wa mguu mpaka utosi wa kichwa.
28:36 BWANA atakupeleka wewe, na mfalme wako utakayemweka juu yako, kwa taifa usilolijua wewe wala baba zako; nawe huko utatumikia miungu mingine ya miti na mawe. (***2 Mambo ya Nyakati 36***)
28:37 Nawe utakuwa mshangao, na mithali, na dharau, kati ya mataifa yote huko atakakokuongoza BWANA.
28:38 Otapanda mbegu nyingi shambani, lakini utavuna haba, kwani nzige watakula mimea yako.
28:39 Utapanda mizabibu na kuitengeza, wala hutakunywa divai yake, wala kuchuma zabibu zake kwani zitaliwa na buu.
28:40 Utakuwa na mizeituni katika mipaka yako yote usijipake mafuta yake; kwa kuwa mizeituni yako itapukutika.

28:41 Utazaa wana na binti, lakini hawatakuwa wako wewe; kwa sababu watakwenda utumwani. (Dan. 1:1-6)
28:42 Miti yako yote, na mazao ya nchi yako italiwa na nzige.
28:43 Mgeni aliye kati yako atapanda juu yako zaidi na zaidi; nawe utashuka chini zaidi na zaidi.
28:44 Yeye atakukopesha, wala wewe usimkopeshe; yeye atakuwa ni kichwa, wewe utakuwa mkia.
28:45 Na laana hizi zote zitakuja juu yako, zitakuandama na kukupata, hata uangamie, kwa kuwa hukuisikiza sauti ya BWANA, Mungu wako, wala kushika maagizo yake na amri zake alizokuamuru;
28:46 Nazo zitakuwa juu yako kwa ishara na ajabu, na juu ya uzao wako milele;
28:47 Kwa kuwa hukumtumikia BWANA, Mungu wako, kwa furaha na moyo wa shukrani, wakati wa ule wingi wa neema alizokupa;
28:48 Kwa hiyo utawatumikia adui zako ambao BWANA atawaleta juu yako, katika njaa, na kiu, na ukiwa uchi, na kwa upungufu wa vitu vyote; naye atakuvika kongwa la chuma shingoni mwako, hata atakapokwisha kukuangamiza.
28:49 BWANA atakuletea taifa juu yako kutoka mbali, kutoka nchi ya mbali, haraka kama arukavyo tai; taifa usiloifahamu lugha yake;
28:50 Taifa la watu wenye uso mkali, ambao hawajali udhaifu wa mzee, wala kumpendelea kijana;
28:51 Nao watakula uzao wa ng'ombe wako, na uzao wa nchi yako mpaka [wewe] utakapokwisha kuangamizwa; wala hatakuachia nafaka, wala divai, wala mafuta, wala ongezoko la ng'ombe wako, wala wana-kondoo wako, hata atakapokwisha kukuangamiza.
28:52 Naye atakuhusuru katika malango yako yote, hata kuta zako ndefu, zenye maboma, ulizokuwa ukiziamini, zianguke, katika nchi yako yote, kila upande; naye atakuhusuru katika malango yako yote kila upande, katika nchi yako yote aliyokupa BWANA, Mungu wako.
28:53 Nawe utakula uzao wa tumbo lako mwenyewe, nyama ya wana wako na binti zako aliokupa BWANA, Mungu wako; katika husuru na katika dhiki atakayokusibu nayo adui yako.
28:54 Hivyo kwamba mtu mume kati yenu aliye muungwana na mtanashati, jicho lake litakuwa ovu juu ya nduguye, na juu ya mke wa kifuani mwake, na juu ya wanawe waliosalia naye;
28:55 Akikataa kuwagawia nyama ya wanawe atakaowala, kwa kuwa hana kitu kilichosalia kwake; katika husuru na dhiki ambayo adui yako atakusibu nayo katika malango yako yote.
28:56 Na mwanamke kati yenu aliye mstaarabu na mwororo, ambaye hatoridhia kukanyaga ardhi kwa unyayo wake kwa umaridadi na ulaini alio nao, jicho lake huyu litakuwa ovu juu ya mume wa kifuani mwake, na juu ya mwanawe, na juu ya binti yake,
28:57 Na juu ya kichanga kitokacho katikati ya miguu yake, na juu ya wanawe atakaowazaa: kwa kuwa atawala kwa siri, kwa sababu ya kukosa chakula, katika husuru na dhiki ambayo adui yako atakusibu nayo katika malango yako.
(***Laana zinazotajwa katika Kumb. 28:49-57 ziliwasibu Wayahudi katika husuru ya Roma dhidi ya Uyahudi kuelekea maangamizi ya Yerusalemu na Hekalu mwaka 70 BK. Tafadhali soma kijitabu “Nini Kilitokea Uyahudi Mwaka 70 BK?” bure katika tovuti yangu https://sayuni.co.tz kwa kupata utondoti zaidi.***)
28:58 Kama hautoshika na kutenda maneno yote ya sheria yaliyoandikwa katika kitabu hiki, upate kuwa na hofu juu ya jina hili tukufu na lenye kutisha, BWANA MUNGU WAKO;
28:59 Ndipo BWANA atakapoleta juu yako majanga makuu na ya ajabu, na pia juu ya uzao wako, magonjwa makubwa na ya muda mrefu.
28:60 Naye ataleta maradhi yote ya Misri juu yako, uliyokuwa ukiyaogopa; hayo yataambatana nawe.
28:61 Tena BWANA atakupiga na kila ugonjwa, na kila tauni ambayo haijaandikwa katika kitabu hiki cha sheria, hata utakapoangamizwa.
28:62 Nanyi mtasalia wachache katika idadi, ninyi mliokuwa mfano wa nyota za mbinguni kwa wingi; kwa kuwa hukuisikiliza sauti ya BWANA, Mungu wako.
28:63 Tena itakuwa, kama vile BWANA alivyokuwa akifurahi juu yenu kwa kuwatendea mema na kuwafanya kuwa wengi, ndivyo atakavyofurahi katika kuwaangamiza na kuwafanya si lolote; nanyi mtang’olewa [kutoka] katika hiyo nchi mwingiayo kuimiliki.

28:64 BWANA atakutawanya katika mataifa yote, tokea ncha hii ya dunia hata ncha hii ya dunia; nawe huko utatumikia miungu mingine usiyoijua wewe wala baba zako, nayo ni miti na mawe.
28:65 Na katika mataifa hayo hutapata pumziko lolote, wala unyayo wa mguu wako hautatulia; bali BWANA atakupa huko moyo wa kutetema, na macho ya kuzimia, na huzuni moyoni mwako;
28:66 Na uhai wako utakuwa mashakani mbele yako; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutakuwa na amani maishani mwako;
28:67 Asubuhi utasema, Laiti ingekuwa jioni! Na jioni utasema, Laiti ingekuwa asubuhi! Kwa sababu ya kile kitakachotia hofu moyoni mwako, na kile kitakachoonekana na macho yako.
28:68 BWANA atakurudisha tena Misri kwa merikebu, kwa ambayo nilikwambia hutaiona tena; nanyi huko mtauzwa kwa adui zenu kuwa watumwa na wajakazi, wala hakuna atakayewanunua.

AGANO JIPYA lilithibitishwa na BWANA Yesu ***kati ya Mungu na watu wengi*** katika Luka 22:20, Matt. 26:28, Waebrania 9:15, nk.

26:27 Akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akinena, kunyweni hiki chote;
26:28 Maana hii ni ***damu yangu ya agano jipya***, inayomwagika ***kwa ajili ya wengi*** kwa ***ondoleo la dhambi***. Matt. 26:27-28

22:20 Vivyo hivyo na kikombe baada ya kula, akinena, Kikombe hiki ni ***agano jipya*** katika damu yangu, inayomwagika ***kwa ajili yenu***. Luka 22:20

9:15 Na kwa sababu hii ***Yeye ni mdhamana wa agauo jipya***, ili kwa njia ya kifo [chake], kwa kukomboa makosa yaliyotendwa katika agano la kwanza, ***wateule*** waweze kuipokea ahadi ya urithi wa milele.
9:16 Maana ili agano la urithi (wosia) litekelezwe, lazima [kwanza] kuwe na kifo cha aliyelifanya.
9:17 Kwa maana wosia una nguvu baada ya kifo cha mwusia; vinginevyo hauna nguvu kabisa wakati mhusika angali hai. Waebr. 9:15-17

***Tazama vizuri misemo “kwa ajili ya wengi”, “ondoleo la dhambi”, “kwa ajili yenu”, na “wateule”.*** Kuanzia hapo, hakuna tena dhabihu kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

Ndugu Mkristo, umesoma mwenyewe, kutoka katika Biblia, ahadi ya Yahweh Mungu, aliyeumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo, kwamba ikiwa utajifunza, utafuata, na kutimiza amri zake, Yeye mwenyewe atahakikisha kwamba utapata neema katika maisha yako. Shughuli zako za kiuchumi zitafanikiwa, uzao wako utaongezeka na utaneemeka; utakuwa na afya njema; utaishi kwa usalama; atakayethubutu kukushambulia atapigwa na BWANA mwenyewe. Nk. Kwa hakika kuna kanuni nyingine ndani ya Biblia ambazo utapaswa kujifunza na kuzifuata zinazohusiana na kilimo, uchumi na biashara, taratibu za kuitunza ardhi, mifugo, mfumo sahihi wa utawala, familia, ndoa, ibada, huduma kwa Wakristo wenzako, zaka, kusaidia masikini, nk. Chunga dhidi ya hukumu na adhabu iliyowakumba Israeli: “Kwa sababu hii nawaambieni, ya kwamba ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, na watapewa taifa lingine wenye kuzaa matunda yake” (Matt. 21:43). Hili la ufalme kupokwa kutoka mikononi mwa taifa la Israeli lilitokea mwaka 70 BK. Tahadhari na watu wanaofundisha kwamba Mkristo hahusiki na amri za Agano la Kale.

Hatma ya maisha ya Mkristo, hapa duniani na baada ya maisha ya hapa duniani, iko katika mikono ya Mkristo mwenyewe. Katika maisha yako hapa duniani, ukiona unaingia katika vikwazo vya kiuchumi, kiafya, kiusalama, nk, basi kuna sababu mbili tu: Mungu anakupima imani yako (mfano Ayubu) au Mungu anakuadhibu kwa sababu zilizoorodheshwa hapo juu. Basi! Asikudanganye mtu yeyote anayejiita nabii, mchungaji, mtume, nk, kwamba yeye ana “upako” utakaoondoa ‘pepo, balaa, laana, mizimu,’ uchawi, umasikini, ugonjwa, unaokutatiza katika maisha yako. Hao ni waongo. Hakikisha mwenyewe kwa kusoma Biblia yako. Kwa hakika, katika Biblia kuna mifano ya mitume na manabii walioponya watu magonjwa. Lakini kipawa hicho kilitolewa na Mungu katika

vipindi mahususi tu; na kwa majira yetu ya sasa, hakuna tena kipawa hicho, kwani kimekabidhiwa kwa Kanisa kwa ujumla; uweza mkuu wa sala na maombi ya Wanakanisa, hususan wazee wa kanisa (Yakobo 5:13-20)

5:13 ***Kuna yeyote kwenu anateseka? Na aombe.*** Kuna yeyote ana furaha? Na aimbe zaburi.
5:14 ***Kuna yeyote kati yenu hajiwezi? Na awaite wazee wa kanisa wamwombee, wakimpaka mafuta katika jina la Bwana.***
5:15 ***Na maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo, na Bwana atamwinua; na kama ametenda dhambi, atasamehewa [dhambi hizo].***
5:16 Ungameni makosa yenu kila mmoja kwa mwenzake, ***na muombeane, mpate kuponywa***. Kuomba kwa mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.
5:17 Eliya alikuwa mwanadamu mwenye hisia sawa na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe: na mvua haikunyesha juu ya inchi muda wa miaka mitatu na miezi sita.
5:18 Akaomba tena, mbingu zikatoa mvua, inchi ikazaa matunda yake.
5:19 Ndugu zangu, ikiwa mwenzenu amepotoka kutoka msitari wa kweli, na mtu mwingine akamrejesha;
5:20 Ajue va kuwa veve amrejeshaye mwenye dhambi kutoka katika njia ya upotovu, ataiokoa nafsi ya mtu yule na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.

Soma vizuri, maandiko yanasema ita wazee wa kanisa, na hao ndio watakaompaka mgonjwa kwa mafuta na kumwombea; siyo jamaa mmoja aliyesimama “madhabahuni” anayejiita “nabii”! Leo hii hakuna manabii wala mitume (1Wakor. 13:8-10). ***Kila Mkristo ni kuhani*** (1Pet. 2:9-10; Ufu. 1:6; 5:10):

2:9 Bali ninyi ni uzao mteule, ***makubani wa kifalme***, taifa takatifu, watu wa kipekee; mpate kutangaza sifa zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake adhimu;
2:10 Ninyi ambao hapo kabla hamkuwa taifa, bali sasa ni taifa la Mungu: hamkuwa na rehema, bali sasa mmepata rehema.

Soma 1Wafalme 22:19-22
22:19 Mikaya akasema, Sikia basi neno la Bwana; Nalimwona BWANA ameketi katika kiti chake cha enzi, na jeshi lote la mbinguni wamesimama upande wa mkono wake wa kuume na wa kushoto.
22:20 BWANA akasema, Ni nani atakayemshawishi Ahabu, ili akwee Ramoth-Gileadi akaanguke? Basi huyu akasema hivi; na huyu hivi.
22:21 Akatoka pepo, akasimama mbele za Bwana, akasema, Mimi nitamshawishi.
22:22 BWANA akamwambia, Jinsi gani? Akasema, Nitaondoka, ***na nitakuwa pepo wa uongo kinywani mwa manabii wake wote.*** Akasema, Utamshawishi, na utafanikiwa pia; ondoka ukafanye hivyo.

Na kuna hii pia:

2Wathess. 2:9-12 (kutoka KJB)
2:9 [Yeye] ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa ***utendaji kazi wa Shetani***, ukiambatana na ***uwezo, na ishara na ajabu zote za uwongo,***
2:10 Na katika ***ghiliba zote za udhalimu [zinazoelekezwa] kwa wapotevu***: kwa sababu hawakukubali kuipenda kweli, wapate kuokolewa.
2:11 Kwa hiyo ***Mungu atawaletea ghiliba ya nguvu, ili wauamini uwongo***,
2:12 Na watahukumiwa wote wasioamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu.

Hivyo tunaona hapa kwamba katika kuwaadhibu watu waovu, Mungu anaamua kumruhusu Shetani awapatie baadhi ya watu kiasi fulani cha uweza wake mkubwa tu (siyo mkuu!) ili watu wasiopenda ukweli wafichuliwe na waangamizwe. Tunaona pia kwamba Shetani na pepo wake wote wana

uweza wa kutenda miujiza. Hivyo ***kutenda miujiza si kipimo cha Uchamung***u; utawajua Wachamungu kwa matunda yao mema.

Na hii:

Matt. 24:24
24:24 Kwa maana watatokea Kristo wa uwongo, na manabii wa uwongo, nao ***wataonyesha ishara kubwa na maajabu***; wapate kuwapotosha, kama yumkini, hata wateule.

Kutoka kwa mafundisho ya Paulo kwa Timotheo, tunaona hili:

2Tim. 3:10-15
3:10 Bali ninyi mmeyajua mafundisho yangu kikamilifu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na ustahamilivu, na upendo, na subira,
3:11 Tena adha na mateso yaliyonipata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra; ***kila namna ya adha niliistahimili: naye Bwana akaniokoa katika yote***.
3:12 ***Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya uchamungu katika Kristo Yesu watateswa***.
3:13 Lakini watu waovu na wapotoshaji wataongezeka katika uovu wao, wakidanganya na wakidanganyika.
3:14 Bali wewe endelea katika yale uliyofundishwa na kuhakikishiwa, kwa maana unajua ni nani ambaye ulijifunza kwake,
3:15 Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, yawezayo kukupa hekima hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu.

BWANA Yesu alisema, Mtawajua kwa matunda yao (Matt. 7:15-23). Hivyo usiridhike tu na matendo yao ya ajabu, ya miujiza. Tumeona kwamba hata Shetani anaweza kutenda miujiza. Miujiza inayokubalika inatoka kwa Mungu pekee. Chunguza mafundisho yao pia. Mafundisho yanapaswa kuendana na Biblia, na yanapaswa kuambatana na nukuu za aya za Biblia. Chunguza kama ni kweli mitume walisema kile anachodai mwalimu wako. Hili ni jukumu lako (Matendo 17:11). Chunguza maisha yao ya Kikristo; chunguza kama huduma yao imekaa kibiashara zaidi, nk. Halafu ndiyo uamue kuwafuata, au la. Yeye ajionaye amesimama, na achunge asianguke (1Wakor. 10:12)!

Imeandikwa na Respicius Kilambo Luciani
Wa tovuti https://sayuni.co.tz
Morogoro 0679900814